Repoti Fupi

# Kompyuta Wilaya ya Kinondoni

## Muhstasari wa Mradi wa Utumiaji

**Anne-Marijke Podt, Veronica Igoko, Denise Senmartin**

**Muhustasari huu unaeleza kilichojifunzwa kutokana na moja ya miradi inayofadhiliwa wa IICD. Muhustasari huu unawalenga watendaji kwenye taaluma ya kompyuta wanaopenda kujifunza kutokana na uzoefu uliotokana na mradi huu pamoja na mashirika yatakayopendelea kutekeleza jambo la kufanana na hili.**




**Muhustasari huu ni matokeo ya zoezi la tadhimini iliyofanywa na mradi kwa miaka michache kwa msaada wa IICD pamoja na mtadimini mzawa. Mfumo wa tadhimini ulijumuisha kwa upande mmoja dodoso zilizojazwa na watumiaji (watumiaji wote ama sampuli) wa mradi kila mwaka na kufuatiliwa na uchunguzi wa data zitokanazo na dodoso, zilizohusu:maelezo mafupi ya watumiaji, matumizi na kadhalika, na taadhira ya mradi. Kwa upande mwingine, palikuwepo mikutanao ya vikundi lengwa iliyohudhuriwa na wafanyakazi wa mradi, ili kuakisi na kutafakari data na kujadili mafanikio, changamoto na fumbuzi.**

**Zaidi ya mafunzo yatokanayo na tadhimini ya data na majadiliano, kuna mengine zaidi yaliyojitokeza kwa miaka mingi yaliyojumuishwa katika muhustasari huu. Muhustasari huu umechanganuliwa/ umefafanuliwa kwa ushirikiano wa wabia wa mradi, yaani Manispaa ya Kinindoni. Wafanyakazi wa mradi na wafanyakazi wa IICD wako tayari kila wakati kufafanua zaidi ama kujibu maswali mahsusi yaliyosalia hata baada ya wewe kusoma maelezo haya mafupi. Kwa ufahamu zaidi kuhusu IICD, tafadhali rejea ukurasa wa mwisho.**

### Maelezo kuhusu nchi na mahitaji makuu ya maendeleo

Ikiwa karibu nusu ya idadi ya watu wanaishi chini ya kiwango cha umasikini, Tanzania iko katika daraja la chini sana kwa kutumia kielelezo cha maendeleo ya binadamu kilichotayarishwa na UNDP. Katika juhudi za kuongeza uzalishaji na kuwavutia wawekeshaji wa kigeni, serikali imeamua kuendeleza sera ya kutopendelea/kutobagua na kutoingilia pamoja na udhibiti wa kutoa madaraka mikoani kwa miaka ishirini iliyopita.

Mradi *"Utumiaji wa Kompyta wilayani Kinondoni"* ni matokeo ya mkutano wa kitaifa was TEHAMA (Teknologia ya Habari na Mawasiliano) ulioitishwa na IICD Dar es Salaam (Jiji kubwa nchini) Julai 1998, kuwakutanisha watu mbalimbali kwenye meza moja mviringo. Utafiti wa awali uliofanya kuhusu mkutano huo uligundua kwamba shughuli mbalimbali zifanyazo na ofisi ya mkuu wa wilaya hazikuwa na ufanisi na palikuwa na uzembe. Mapungufu ni pamoja na ufinyu wa uwazi kwa sababu ya

**Takwimu za Tanzania**

| | |
|---|---|
| Eneo (sq. km): | 947.3 elfu |
| Idadi ya watu: | 39.5 mln |
| Matarajio ya muda wa kuishi: | 52 |
| Andikishi katika shule, msingi: (% halisi) | 97.8% |
| Kielelezo cha maendeleo ya binadamu UNDP (kati ya nchi 177): | 159 |

**Upatikanaji wa tekinologia ya mawasiliano kwa kila watu 1000**

| | |
|---|---|
| Watumiaji wa simu za kiganja: | 52 |
| Watumiaji wa Intaneti: | 9 |
| Wenye kompyta (PC): | 11 |

**Data ya mradi**

Sekta: Utawala bora

| | |
|---|---|
| Namba ya watumiaji | 500 |
| Namba ya wanufaikaji: | 6000 |

Kundi(ma) lengwa:
Madiwani na wafanyakazi manispaa
Wakaazi wa manispaa Kinondoni: 1,088,867 (sensa 2002)

***Mchoro 1:*** *Chanzo: World Bank - ICT at a Glance, 2005.*




***Mchoro 2:*** *Kipindi cha Mradi Kinondoni*

kukosekana kwa mtiririko huru na upatikanaji wa taarifa. Kukosekana kwa mtiririko huru na upatikanaji wa taarifa, kuliwafanya wenye madaraka manispali washindwe ama kufanya maamuzi sahihi au kusimamia mandeleo husika. Hii imelemeza na kudhoofisha mikakati yenye maono, na matokeo yake ni utumiaji wa rasilimali bila ufanisi.

Kwa hiyo, madhumnuni ya mradi ni uboreshaji utawala wilayani Kinondoni, moja ya mamlaka za manisipaa Dar es salaam, kupitia utumiaji wa TEHAMA.

Wakati wa utekelezaji wa mradi Kinondoni, pia juhudi za kuanzisha utumiaji wa TEHAMA kwa ajili ya uongozi/utawala (mitaa) Tanzania ilijulikana, juhudi hizo ni kama za UNDP kukusanya data kwa ajili ya databezi/kaida ya taifa na mfumo wa shughuli za kifedha katika taasisi za serikali. Hata hivyo, juhudi zote hizo zilibuniwa na kutekelezwa kwa maamuzi toka juu kuja chini, na hakuna hata mojoa iliyoleteza utumiaji TEHAMA katika mapana na kwa taasisi nzima.

Kinondoni ni moja ya wilaya tatu za mkoa wa Dar es Salaam. Ina jumla ya wadi 27 zenye zaidi ya wakazi millioni moja. Manispaa ina wafanyakazi 6000 na ilichaguliwa kwa ajili ya mradi kwa sababu ya maskani ya COSTECH (Tume ya Sayansi na Teknologia), moja ya mbia mtekelezaji mradi.

## Kundi lengwa na makusudi ya mradi

Walengwa wa mradi ni wafanyakazi wa manispaa, ambao wanaadhiriana/ wanaingilina na taarifa moja kwa moja. Ni dhahiri, wananchi wamefaidi mradi pia kwa sababu taarifa zilizotolewa na wafanyakazi wa manispaa ni sahihi zaidi na haraka kupatikana, kwa mfano, taarifa za hati za aridhi.

Watumiaji wa mradi wa Kinindoni ni makundi mbalimbali wakiwepo mameneja, wafanyakazi watawala, mafundi na wasaidizi. Wafanyakazi mafundi na wasaidizi ni theluthi mbili za walengwa wote.

Usawa wa kijinsia haikuwa ni hoja katika mradi, jinsia zote zilivinjari asilimia 50 kwa miaka yote. Hata hivyo wanawake walikuwa na uwakilishi mkubwa katika kundi la waunga mkono (75 % ya wanawake). Umri wa walengwa pia umetawanyika hass, asilimia 73 wakiwa na umri kati ya miaka 31-50. Kwa upande wa elimu, zaidi ya nusu walikuwa na elimu ya juu (elimu baada ya kidato cha sita) (wastani wa asilimia 60 kwa miaka yote) ingawaje namba hii imekuwa ikipungua jinsi miaka inavyokwenda.

Tangu mradi uanzishwe, watumiaji wanaoshiriki katika mradi waliulizwa motisha wao wa kushiriki katika mradi (ingawaje wote walikuwa sehemu ya mradi kwani idara zao zilihusika, swali lililenga kichocheo binafsi). Wengi walionyesha kuwa walitaka kujifunza kuhusu TEHAMA, na la muhimu zaidi waliashiria walitaka kutumia maarifa hayo kuleta ufanisi katika manispaa. Kwa maneno yao “kuendeleza ufanisi wa kazi kwa kurahisisha kutoa kazi/ripoti sahihi kwa muda muafaka na gharama nafuu” na ”Kuweka rekodi sahihi za umiliki wa aridhi, kupunguza ugomvi na kuboresha mapato kupitia kodi ya aridhi”.

La muhimu zaidi katika mradi ni mtazamo wa kuanzia chini juu katika kila jambo. Wafanyakazi wa kawaida walihusishwa katika kutambua aina ya habari/taarifa walizohitaji na kuendeleza matumizi ya manufaa ya TEHAMA kwa kazi zote.

Awamu ya majaribio ya mradi ilianza mwaka 2000 iliainisha maeneo matatu kwa ajili ya matumizi ya kompyuta: elimu, afya na usajili wa uzazi, ndoa na vifo. Huduma ya TEHAMA hasa imerahisisha uwekaji wa rekodi, uwazi juu ya ushuru/ makusanyo ya ushuru na matumizi, bajeti, kushirikiana taarifa miongoni mwa maidara na majibu ya haraka kwa usimamizi wa migogoro ya aridhi. Mfumo wa kupata habari za kigeografia (GIS) ulitumika kwa data za hati za aridhi, ambazo ziliwezesha kukisia na ukusanyaji wa ushuru wa rasilimali.

Vifuatavyo ni vipengele muhimu vya mradi:

- Data zilizotengemaa – na mtiririko wa kazi ukizingatia mahitaji katika ngazi ya uendeshaji
- Uboreshaji wa uhifadhi na upatikanaji wa data
- Kutengemaa kwa uchananuzi wa data na kufanya maamuzi katika ngazi ya wilaya kwa kutegemea data kutoka sekta husika (elimu, afya, aridhi).

Kipengele kingine muhimu cha mradi ilikuwa kuzihusisha serikali za mitaa kuhusu uwezekano wa kutumia TEHAMA ili kutegemeza utendaji.

Kwa sababu ya mipango bora, mawasiliano yaliboreshwa na uhusishaji wa taarifa, malengo ya manispaa kutoa huduma bora kwa jamii, na wakati huo huo maboresho ya mapato manispaa yalifanikiwa.

## Taadhira ya Mradi

Matokeo ya utumiaji kompyuta katika wilaya umepimwa takribani miaka mitano sasa, yakitoa picha nzuri ya maendeleo ya mradi kwa muda huo. Kuanzia mwaka 2003, mradi ulikusanya dodoso 180 za watumiaji wa mradi (wafanyakazi wa manispaa).

Mafanikio hapa yalipimwa kwa kuwauliza watumiaji mradi kwa kujibu maswali kupitia skeli ya pointi 7 (Sikubaliani kabisa mpaka Nakubaliana sana) na baadaye kujumuisha kauli zote katika tafsiri tano: Mwanko, Kuwezeshwa, Taadhiria kimfumo, Taadhiria kiuchumi, na taadhiria hasi. Data iliyokusanywa pia iliangalia maelezo mafupi kuhusu watumiaji, kuridhika kwao na utumiaji wao wa mradi.

Taadhira kimfumo ni ishara kuwa pamekuwepo ukuaji kwa muda wa miaka sasa inayojumuisha kujihusisha na matokeo ya mlolongo wa kutoa madaraka, kuandika ripoti, uwazi wa serikali na uboreshaji wa huduma manispaa. Hata hivyo, kama data inavyoonyesha, mlolongo wa kupata matokeo halisi katika mfumo mzima umekuwa ni mrefu.




***Mchoro 3:*** *Taadhira Kinondoni.*
**Kwa sababu za mabadiliko kwenye dodoso, data ya 2007 ilichanganuliwa kipekee iliosababisha matokeo tofauti. Pia, 2007 ilikuwa mara ya kwanza kupima taadhira hasi.*

Kukua kwa taadhira ya mfumo unungwa mkono na madai kutoka kwa wafanyakazi wa manispaa kuwa malalamiko ya wananchi ya kuhusu huduma zao yamepungua kutokana na wao kutumia vizuri TEHAMA. Hili pia limedhibitishwa na maoni ya watumiaji kuwa: "mradi umemaliza rushwa, unaweka kumbukumbu kwa muda mrefu na umepunguza sana utumiaji wa makaratasi" na "kumbukumbu zinaweza kuhifadhiwa na kupatikana tena, kuhaririwa, na kunakilishwa tena". Utaratibu/mpangilio wa huduma za manispaa zimekuwa nzuri zaidi, matokeo yake ni huduma kupatikana haraka zaidi. Shukurani ziende kwa GIS, kwani wananchi hawana haja tena ya kungojea muda mrefu kabla ya kupata melezo ya jumla kuhusu kodi ya aridhi au kiwanja kwenye aridhi iliyo chini ya manispaa, kwa sababu taarifa zinapatikana bila shida.

Malalamiko ya wateja yamepungua sana na uwazi umeongezeka. Tovuti ya manispaa sasa ina sanduku la maoni na madiwani wote sasa wana anwani zao za barua pepe ili wananchi waweze kuwatumia fikra zao, maswali na maoni. Anwani hizo zimewezesha kupata shukrani nyingi kutoka kwa umma, ikiwa ni pamoja na matumizi, kwa mfano, mkaazi mmoja wa Kinondoni aliyetaka huduma za usafi zaidi katika eneo lake akidhibitisha kwa kumtumia diwani picha inayoonesha lundo la takataka mtaani kwake.

Huduma za TEHAMA pia zimepelekea mapato makubwa zaidi ya manispali. Mapato yameongezeka kwa asilimia 88 tangu huduma hizi zianzishwe mwaka 2005. Kiasi cha ongezeko la mapato kimerudi kwenye idara ya TEHAMA ili kuwezesha huduma kuendelea kuboreshwa.




***Mchoro 4: Bango za matangazo Kinondoni**. Kabla, matangazo ya biashara yalibandikwa bila utaratibu katika mabango ya manispaa. Sasa, madiwani wanaweza kufuatilia kila bango manispaa, mfano mwingine wa jinsi mapato ya manispaa yalivyoongezeka.*

Ikiwa na taadhira hasi isiyokusudiwa ya mradi, watumiaji wameona ukweli kuwa, 'madadiliko ya teknologia yamevuruga kwa muda mfupi jinsi ya utendaji kazi wa kila mmoja". Haswa wafanyakazi wa ngazi za juu na wafanyakazi wenye kiwango kikubwa cha elimu, wakiwa na matarajio makubwa ya teknologia mpya haswa, kasi na ufanisi; walikerwa na teknologia kushindwa au kutokuweza kutoa majibu haraka ilivyotarajiwa.

La kupendeza, kwa miaka sasa mradi unaonekana kuwanufaisha wanaweke zaidi kuliko manaume, pia watu wenye kiwango kidogo cha elimu nao walinufaika zaidi kuliko wenye elimu ya sekondari na haswa wenye elimu ya juu. Hili lilipojadiliwa kwenye mikutano ya vikundi lengwa (focus groups) ilielezwa kuwa wanawake mara nyingi hufanya kazi za nafasi za chini katika mashirika (makatibu muhtasi, na kazi nyingine za usaidizi), ambalo linaungwa mkono na uwiano mkubwa kati ya jinsia na kiwango cha elimu. Katika nafasi hizo, wanawake ndio wao hutendea kazi za TEHAMA, wakati mabosi wao (wanaume) mara nyingi wana shughuli nyingi nyingine na sio kutumia kompyta. Haswa miaka ya hivi karibuni, wanawake wamekuwa na uwakilishi mkubwa kwenye hii mikutano ya vikundi lengwa kwa idadi na ushiriki katika majadiliano. Majadiliano pia yaliweka wazi kwa nini uwezeshaji ulionekana mkubwaa: wanawake walidai TEHAMA iliwafanya wajisikie vizuri kuwa na ujuzi na ustadi ambao hata mabosi wao wakati mwingine walikuwa hawana.

### Yaliyojifunzwa

Ilichukua muda kufungamanisha (integrate) TEHAMA katika manispaa na kuna mambo mawili yaliyojifunzwa yanayosisitizwa. Usimamisi wa mabadiliko ni kipengele muhimu cha mradi kama huu na hatua mbalimbali zilizochukuliwa ili kulishughulikia. Mosi, mafunzo ya TEHAMA yaliandaliwa kwa kundi kubwa na pili, warsha ya siku mbili ilifanyika kuwaleta pamoja wadau wote kuchunguza na kupendekeza nafasi ya TEHAMA katika manispaa. Hii iliandaa njia ya

kukubalika kweli TEHAMA na matumizi yake katika manispaa. Washiriki wa mafunzo na warsha waligundua umuhimu wa taarifa kwa ajili ya kazi zao na waliona TEHAMA kama 'wajibu' kushirikisha wengine. Na hata mpaka sasa, mpango mkuu wa TEHAMA na kuendeleza mafunzo kazini kwa wafanyakazi limekuwa jambo la kukubaliwa na kufaa kwa mzigo wa kazi manispaa.

Usimamizi wa mabadilikoilikuwa mada muhimu wakati wa warsha ya mwanko (awareness) na uruduvishaji iliyofanyika mwaka 2006 na 2007 kwa ajili ya serikali za mitaa. Warsha ya uruduvishaji ya mwaka 2006 ilihudhuriwa na manispaa 13 mbalimbali za Tanzania. Katika warsha ya kuongeza mwamko, iliangalia kwa upana mada zaidi ya Kinondoni ikiwa ni pamoja mada na miradi ya kilimo na afya, pamoja na uongozi wa mitaa, ikilenga zaidi meneo ya Magu na Mwaza, karibu na ziwa Viktoria.

Pili, njia wazi za mawasiliano na mwongozo vilihitajika, pamoja na upangiaji wa majukumu. Utumiaji kompyuta Kinondoni ulimaanisha kushirikiana taarifa/habari, ambayo ilihitaji mawasiliano. Mambo muhimu ya kufanyia kazi yalikuwa kujaribisha na kuyapa kipaumbele mabadiliko, kuwasiliana na kwa uwazi, kupeana majukumu na kuimarisha mabadiliko. Sehemu moja muhimu ya usimamizi wa mabadiliko ilikuwa pia kuondoa mashaka kuwashawishi wakuu wengi wa idara na huduma kukubaliana na utendaji mpya wa kazi na kubadili wajibu wao kwa mujibu. Menaja mzuri wa mabadiliko, ambaye kwa suala la Kinondoni alikuwa meneja wa IT (teknologia ya habari [TEHA]), ni sharti muhimu kwa mfumo mkubwa kisiasa kama manispaa ili kufanyika mabadiliko hayo.

## Changamoto

Changamoto kubwa sana ya mradi kwa sasa inahusiswa na mafunzo. Ingawaje kundi kubwa la watu limepata mafunzo, mafunzo zaida, haswa kwa watumiaji wa mwisho (yaani wafanyakazi wa manispaa) bado yanahitajika. Mapato ya ziada yalitumika kukodisha watendaji kiufundi zaidi wa TEHAMA, hata hivyo kwa jinsi maidara yalivyohitaji kufaidika na mapato ya ziada, fedha hiyo haitoshi kutayarisha mafunzo makubwa. Kwa sasa manispaa ina wafanyakazi 6000 na kompyuta 300, zilizonunuliwa na manispaa yenyewe. Karibu watumiaji 500 wa kompyuta hizo wameshapata mafunzo kwa sasa, lakini baadhi ya hawa watumiaji sio wafanyakazi tena wa manispaa. Hiki kiasi cha wanaokuja kujaza nafasi kinaashiria kuwa juhudi za kuwa na mafunzo ziwe endelevu.

Haswa mafunzo yanahitajika kwa wafanyakazi wa kada ya chini, kama matibu muhstasi. Kama ilivyokuwa wazi kutokana na data za tathimini na majadiliano toka kundi lengwa, zaidi ya mameneja (waliofunzwa), makatibu muhutasi (wasio na mafunzo) ndio mara kwa mara ambao lazima wafanye kazi kwa kutumia TEHAMA. Fedha zaidi zinahitajika kwa mafunzo ya hawa watumiaji wa huduma manispaa.

Changamoto nyingine ni msaada unaotolewa kwa wafanyakazi wa Teknologia ya habari (TEHA). Hawa wakiwa wanne tu, ni wachache mno. Katika mkutano wa kikundi lengwa 2007, msaada wa kifundi (ama ufinyu wake) ilikuwa ni mada muhimu zilizojadiliwa. Watumiaji walidai ilikuwa ngumu kuwafikia na wakati mwingine kuelewa lugha yao ya kifundi inayotumiwa na mafundi hao. Hawa mafundi walishindwa kabisa na wingi wa maombi ya msaada, mara nyingi kwa matatizo mengi ya msingi yanayohusika na ukosefu wa mafunzo kwa watumiaji na mwisho kama ilivyoelezwa mwanzo. Wakati wa mkutano wa kikundi lengwa, mawazo mengi yaliwasilishwa (kama vile tangazo la jinsi ya kutatua matatizo madogo kwenye ofisi za wafanyakazi) na swali moja muhimu lilikuwa ni: Je IICD yaweza kutusaidia kuratibu deski la msaada kwa TEHAMA? Kama jibu, mwezi Novemba 2007 mshauri toka InterAccess (moja ya wabia binafsi wa IICD) mwenye usoefu katika mwenendo wa kazi za TEHAMA kwenye mfumo alikaa kwa wiki Kinondoni akifanya kazi na kushughulikia hoja kama:

- Jinsi ya kusajili simu katika kitabu cha usajili
- Jinsi ya kukadiria muda utakaohitajika kutatua na kuwasilisha hilo kwa mteja
- Jinsi ya kuratibu kazi za wafanyakazi wa manispaa
- Jinsi ya kuhakikisha kila idara ina mtu muhimu, ili wat wa idara wamwone yeye kwanza kabla ya fundi.

Changamoto za kiufundi bado zimebakia bila ufumbuzi. Mradi bado unapambana kuhifadhi data katika seva (server) namna ya kupanga vizuiamoto (firewalls) kwa ajili ya kompyuta zote, na hitaji la kuchunguza virusi vya kompyuta kwa kujiendesha yenyewe kwa kutumia bidhaa pepe/bidhaa laini ya kuondoa virusi.

## Hatua nyingine na Mipango ya baadaye

Mradi umekuwa kama kielelezo cha mafanikio ya matumizi ya TEHAMA yaliyofuata mlolongo wa mawazo kuanzia chini kwenda juu katika utawala. Kwa matrajio ya muda mrefu, mtazamo huo utakuwa muhimu kwa uwezeshaji kupeleka madaraka ngazi za chini kwa nchi kubwa kama Tanzania. Ongezeko la uwazi na uwajibikaji yataboresha mifumo ya demokrasia. Faida ya ziada ya mradi ilyoonekana kwa serikali za mitaa sehemu nyingine za Tanzania ni ushahidi tosha wa dhamani ya njia hii. Halimashauri ya manispaa ya Kinondoni inasifiwa zaidi na mamlaka nyingine (ndani na kimataifa) na zinataka kushirikiana nao uzoefu wao. Juni 2007 mtandao wa maendeleo ya TEHAMA kitaifa Tanzania (SWOPNET) waliandaa warsha ya TEHAMA huko Mwanza, mkoa katika kanda ya ziwa, iliyolenga kushirikiana maarifa yaliyojifunzwa kutokana na uzoefu wa Kinondoni na miradi mingine ya TEHAMA. Serikali za mitaa za Mwanza na Magu zilihudhuria na wanajumuia 10 wa manispaa ya Mwanza baadaye waliamua kufanya ziara ya mafunzo Kinondoni kujionea mradi ukitekelezwa na kutumia maarifa hayo kuendeleza mikakati yao wenyewe ya TEHAMA.

Manispaa nyingine ambazo, kwa misukumo yao wenyewe, zilizo tembelea mradi mwaka 2007 ni pamoja na Morogoro, Tanga, Dodoma na Zanzibar. Mnamo Oktoba 2007, Veronica Igoko, mratibu wa TEHAMA Kinondoni, alieleza mafanikio ya Kinondoni wakati wa warsha ya eGovernment kwa serikali za mitaa huko Nairobi, Kenya. Mradi pia umeelezwa kama mrafo wa Tanzania kuendeleza eGovernance kwenye videoconferences zilizofanywa na Benki ya Dunia.

Kuendeleza zaidi kushirikiana, IICD inasaidia Kinondoni katika majaribio mbalimbali ya kuweka katika mfumo matokeo ya mradi, kwa njia ya uchapishaji na njia mbalimbali za mawasiliano. Matokeo haya yanaweza kutumika kwa kubadilishana maarifa na kielelezo kusaidia mradi kutafutia zaidi sana fedha ziada inayohitajika.

Kwa sasa, mpango wa mkakati wa TEHAMA unahitaji masahihisho na manispaa pamoja na IICD wanashughulikia. Kwa msaada wa IICD, mpango mkuu uliotayarishwa kwanza utafanyiwa masahihisho na mapendekezo ya kuuboresha yatafikiwa. Baada ya hapao, warsha imepangwa kubadilishana uzoefu na wafanyakazi wa Kinondoni pamoja na kikundi muhimu cha washauri/mabingwa ambao wamehusika na mradi kwa muda mrefu. Hawa mabingwa wataelezea uzoefu wao kwa vyuo vikuu Tanzania, wakuu wa shule na washauri. Huku kuhakiki mkakati utaweka kumbu kumbu ya:

- Hali ilivyo (watumishi, uwezo, faida, vikwazo vya utekelezaji, na kadhalika) ukilinganisha na mkakati
- Mambo ambayo yamejifunzwa
- Njia mbeleni (the way forward), haswa kuhusu GIS na usimamizi wa fedha, na kama inawezekana pia kuhusu huduma kwa wateja, elimu na afya.

## Kwa mawasilina yahusuyo mradi


- Ms. Veronica Igoko, Manispaa Kinondoni, msmalangwa@yahoo.com
- Mr. Nic Moens, Country manager Tanzania, IICD, nmoens@iicd.org


## Taarifa kuhusu Muhstasari huu na namna ya tadhimini ya IICD


- Ms. Anne-Marijke Podt, Officer Monitoring and Evaluation IICD, ampodt@iicd.org
- Ms. Denise Senmartin, Officer Knowledge Sharing IICD, dsenmartin@iicd.org


## Kiungo cha Tovuti

- Mshiriki mwenza wa mradi COSTECH - www.costech.or.tz
- Halimashauri ya Manispaa Kinondoni - www.kinondonimunicipality.go.tz
- Repoti Kinondoni 2007 – www.iicd.org/files/2007LearningReportKinondoni.pdf
- IICD: www.iicd.org
- Vyombo vya tathmini kutumia mtandao kwa IICD: www.demosurvey.iicd.org